JARIDA LA MTANDAONI

# AFYA BULLETIN

TOLEO NO. 7 SEPTEMBA-NOVEMBA, 2022

WIZARA YA AFYA

# JENGO LA MAMA NA MTOTO KUHUDUMIA WAJAWAZITO ZAIDI YA 300



SOMA HABARI UK.2



Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi wa Mkoa wa Njombe wakati wa ziara yake mkoni humo kwa lengo la kukagua miradi ya ujenzi wa majengo ya hospitali ukiendele.

## RAIS SAMIA AWATAKA WATUMISHI HOSPITALINI KUFANYA KAZI KWA JUHUDI KUOKOA MAISHA YA WATU

SOMA UK. 5

## NHIF ITAENDELEA KUWEPO NA KUTOA HUDUMA KWA WANANCHI



SOMA HABARI UK.4



## UWEKEZAJI WA RAIS SAMIA SEKTA YA AFYA WAVUTIA NCHI JIRANI KUJA KUJIFUNZA TANZANIA

SOMA UK. 6

## KITUO CHA KUTOLEA MAFUNZO KWA NJIA YA MTANDAO CHA ZINDULIWA TANZANIA



SOMA UK. 7



## TANZANIA KUTOKOMEZA UGONJWA WA USUBI IFIKAPO MWAKA 2030

SOMA UK. 8



*Jengo la Huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya lililojengwa kwa thamani ya Shilingi Bilioni 11*

# JENGO LA MAMA NA MTOTO KUHUDUMIA WAJAWAZITO ZAIDI YA 300

**Mbeya**

**UWEZO** wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya (MZRH) kuhudumia wakina mama wajawazito wanaofika kujifungua utaongezeka kutoka wajawazito 150 hivi sasa hadi kufikia 300 kwa wakati mmoja.

Hatua hiyo ni baada ya kukamilika kwa jengo la kutolea huduma za mama na mtoto ndani ya hospitali hiyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jengo hilo hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan mara baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Jengo la kutolea huduma za Mama na Mtoto katika Kitengo cha Wazazi Meta.

"Hospitali hii itatoka kulaza wakina mama 150 hadi kufikia zaidi 300 kwa kanda nzima, wakina mama watakaokuwa na hali ngumu pia wataletwa hapa," alisisitiza Rais Samia.

Aliongeza "Jengo hili limewekewa miundombinu ya kisasa kuweza kusaidia utoaji wa huduma bora kwa akina mama wajawazito na watoto pamoja na kuweka miundombinu ya kuruhusu wanaume kuwepo katika shughuli hiyo ya kuleta kiumbe duniani.

"Mimi kama mama kazi inayofanywa humu ndani naijua vizuri, naelewa kwamba ni kazi inayohitaji mazingira mazuri sana lakini pia inahitaji faraja na kwa maana hiyo hospitali hii tumeweka vyumba ambavyo mwenza wako atakuwemo humo ndani" alisema Rais Samia.

Alisema Serikali inafanya yote haya ili kuokoa maisha ya mama na watoto huku akisema kuwa uwekezaji huo uliofanywa katika Nyanda za Juu Kusini unafanyika katika maeneo mengine nchi nzima.

Naye, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, alimshukuru Rais Samia kwa kuweka jiwe la msingi katika hospitali hiyo na kumpongeza kwa kuendeleza kazi walioyoianza toka Awamu ya tano ambapo Serikali ilitoa Tsh. Bil. 5 kuanza ujenzi wa jengo.

"Serikali ya Awamu ya Sita nayo imeendeleza ujenzi kwa kutoa Tsh. Bil. 6 kukamilisha ujenzi wa jengo hili ambalo limegharimu Tsh. Bil. 11," alibainisha.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akifurahi mara baada ya kuweka Jiwe la Msingi katika ujenzi wa Jengo la Huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda- Mbeya*



## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI:**
Prof.Abel Makubi
(KATIBU MKUU-IDARA KUU AFYA)

**MHARIRI MKUU:**
Catherine Sungura
(KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI)

**WACHANGIAJI:**
Catherine Sungura
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Rayson Mwaisemba
Abdurkarim Majid
Said Nyaoza

**IMEANDALIWA NA**
Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini-Wizara ya Afya

**MAWASILIANO:**
Wizara ya Afya
Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya

S.L.P 743
40479 DODOMA.
Simu: +255 26 232 3267

**Jikinge, Wakinge Wengine Corona inazuilika**




# UGENI WA MTENDAJI MKUU WA GLOBAL FUND NCHINI TANZANIA

Katika kuendeleza mashirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na wa nje ya nchi, Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Mhe Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa mstari wa mbele ambapo mashirikiano hayo yamekuwa yakileta mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali zenye lengo la kuinua nchi kiuchumi.

Hayo yamedhihirisha hivi karibuni ambapo Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) Bw. Peter Sands aliwasili nchini tarehe 6 Septemba, 2022 kwa ziara ya kikazi ya siku mbili na kukutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ikulu ndogo jijini Dar es Salaam. Ziara ya Bwana Sands imefanyika kufuatia mwaliko alioutoa Mhe Rais Samia wakati wa kikao kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 8 Agosti, 2021.

Rais Samia aliishukuru Global Fund kwa kukuza ushirikiano na Tanzania ambapo kwa miaka 21 iliyopita shirika hilo limekwishaipatia nchi yetu Zaidi ya shilingi Trilioni 6.4 kwa ajili ya kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria pamoja na kuimarisha mifumo ya afya.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan alisema ufadhili wa Global Fund umechangia kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa wa UKIMWI kutoka vifo 100,000 mwaka 2010 hadi kufikia vifo 54,000 mwaka 2021. Kwa upande wa ugonjwa wa Kifua Kikuu, vifo vimepungua kwa asilimia 52 sawa na vifo 56,000 kwaka 2015 hadi kufikia vifo 26,800 mwaka 2021. Mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa kutokomeza ugonjwa wa Malaria ni pamoja na kupungua kwa waliogundulika na ugonjwa huo kutoka watu milioni 7.7 mwaka 2015 hadi watu milioni 4.4 mwaka 2021.

Bw. Sands pia alikutana na kufanya mazungumzo na Mhe Ummy Mwalimu Waziri wa Afya na pia kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya na huduma za afya katika ngazi jamii katika Mkoa wa Pwani. Waziri Ummy alitumia fursa hiyo kuishukuru Global Fund kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri wa Tanzania katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu pamoja na Malaria. Aidha, aliushukuru Mfuko huo kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa afua mbalimbali zinazolenga kukabiliana na magonjwa mengineyo yakiwemo Kifua Kikuu, Malaria, UVIKO-19 ikiwa pamoja na uboreshaji wa mifumo ya sekta ya Afya nchini.

Viongozi hao walijadiliana njia zitakazowezesha ufanisi wa miradi inayofadhiliwa na Global Fund na kujadili afua za kipaumbele zitakazowezesha Tanzania kufikia malengo ya kutokomeza magonjwa matatu pamoja na nchi kujiandaa katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kwa kuboresha mifumo yake ya afya .

Waziri Ummy alisema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imelenga kuboresha ubora wa huduma hivyo kwa kushirikiana na Global Fund, Serikali inatarajia kufikia malengo yake katika mapambano dhidi ya VVU kwa kuwa na afua zilizolenga kuelimisha na kuhamasisha wananchi kutambua mapema hali za afya zao, kuongeza utambuzi wa watu wapya wenye VVU pamoja na kuzuia maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Bw. Peter Sands alipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha Sekta ya Afya nchini na kutoa kipaumbele katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na kuahidi ushirikiano zaidi na kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Tanzania kufikia malengo ya kidunia ya kukabiliana na maradhi hayo.



# NHIF ITAENDELEA KUWEPO NA KUTOA HUDUMA KWA WANANCHI

**Dodoma**

**SERIKAL**i inaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unakuwa imara, endelevu na stahimilivu.

Waziri wa Afya Ummy Mwalimu hivi karibuni alipozungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma.

"NHIF itaendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa kuwa mfuko huo ni moja kati ya mfumo unaotumika katika kuhakikisha huduma za afya zinatolewa nchini," alisema.

Aliongeza "Niwatoe wasiwasi wadau wote wakiwemo wanachama, watoa huduma pamoja na watanzania wote kuwa mfuko wa NHIF utaendelea kuwepo na kutoa huduma kama kawaida kwa wananchi.

"Kwa kuwa mfuko huu ndio umekuwa tegemeo la watanzania wengi hususani wa kipato cha chini, Mfuko huu pia ndio umekuwa tegemeo la vituo vya kutoa huduma za afya nchini," alisisitiza.

Waziri Ummy alisema pamoja na kuwa na wanachama asilimia nane (8) tu ya Watanzania wote, vituo vingi vya kutolea huduma vinategemea mapato kutoka katika Mfuko kwa zaidi ya asilimia 70.

"Ili kuhakikisha mfuko wetu unakuwa endelevu na imara zaidi katika kuwahudumia wananchi tumeona uendelevu wa mfuko huu kuwa unategemea sana ongezeko la wanachama watakaoandikishwa katika Mfuko huu," alisema.

Waziri ummy alibainisha kuwa mfuko huo unahudumia takribani wanufaika milioni 4.8 ikilinganishwa na wanufaika 691,173 waliokuwa wakihudumiwa mwaka 2001/02.

"Hivyo uwepo wa takribani asilimia 99 ya wanachama waliojiunga kwa hiari ambao ni wagonjwa imekuwa ikiongeza gharama za matibabu zinazolipwa na Mfuko.

Alisema imebainika kuwa ili mfuko huo uweze kuendelea lazima hatua stahiki zichukuliwe ikiwemo hatua ya kuimarisha afua za kushughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Alitaja hatua nyingine ni kuongeza idadi ya wanachama, kudhibiti vitendo vya udanganyifu, kudhibiti matumizi ya huduma yasiyo na tija, kupunguza gharama za matibabu nchini na kuwa na Mfumo endelevu wa kuhakikisha Mfuko unakuwa na fedha wakati wote.

"Changamoto kubwa ni uwepo wa kundi kubwa la wananchi wanaojiunga na NHIF kwa hiari ambao, takribani asilimia 99 ni wagonjwa na hatua hii imetokana na kutokuwepo kwa Sheria ya ulazima kwa wananchi kujiunga na Bima ya Afya," alisisitiza.

Hata hivyo, Waziri Ummy aliema kuwa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo itaweka mazingira kwa kila mtanzania kuwa na bima ya afya ili kuwezesha dhana ya kuchangiana gharama za matibabu na hivyo kuwaepusha wananchi katika hatari ya janga la umaskini pindi wakiwa wagonjwa.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu aliwahimiza pia Watanzanzia kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya ili kuweza kupata huduma hata pindi mwananchi anapokuwa hana fedha za kumudu gharama kwa wakati huo.




*Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu*



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimwagilia mti katika jengo la huduma ya Afya kwa mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe.

# RAIS SAMIA AWATAKA WATUMISHI HOSPITALINI KUFANYA KAZI KWA JUHUDI KUOKOA MAISHA YA WATU

**Njombe**

**RAIS** wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amewataka wafanyakazi (watumishi) waliopo hospitalini kufanya kazi kwa juhudi na kuokoa maisha ya watu ili kuwa na jamii yenye afya bora.

Agizo hilo alilitoa hivi karibuni wakati alipotembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe na kukagua ujenzi wa miundombinu iliyojengwa Hospitalini hapo kwa thamani ya Tsh. Bil. 27.

"Wafanyakazi wa hospitali nawashukuru sana, Mungu awatie nguvu muwahudumie wananchi, Mungu amekupanga hapo ili turudishe afya za Watanzania waweze kuingia mashambani, ofisini, waingie maeneo ya kazi tujenge taifa letu," alisema

Rais Samia alisema amesikia changamoto wanazokutana nazo watoa huduma za afya ikiwemo mahitaji ya vitendea na kuwaasa kuchapa kazi huku Serikali ikiendelea kushughulikia changamoto hizo.

"Chapeni kazi, matakwa yenu tunayafahamu ikiwemo mahitaji ya vitendea kazi, tutakwenda kujitahidi kuyatimiza ili muweze kufanya kazi vizuri," alisisitiza.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu katika hospitali hiyo, Rais Samia alisema Serikali inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo inaielekeza Serikali kusogeza huduma za afya karibu kwa wananchi.

"Tulitaka kufanya haya muda mrefu nyuma, kazi za Serikali ni hatua kwa hatua, kipindi hiki tumeweza kufanya haya na tunafanya kwa nchi nzima," alisema Rais Samia



Rais wa Tanzania mhe. Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi wa Mkoa wa Njombe wakati wa ziara yake mkoni humo kwa lengo la kukagua miradi ya ujenzi wa majengo ya hospitali ukiendele.

Awali akizungumza, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kuboresha Sekta ya Afya nchini.

"Kuna kazi kubwa inafanyika Mkoa wa Njombe ikiwemo kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na ya mkoa ambapo tumekamilisha ujenzi wa majengo," alisema Waziri Ummy.

Waziri Ummy alisema ujenzi wa hospitali hiyo ulianza Mwaka 2016 na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 98 huku ukigharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 27.

# UWEKEZAJI WA RAIS SAMIA SEKTA YA AFYA WAVUTIA NCHI JIRANI KUJA KUJIFUNZA TANZANIA

Dar es salaam

UWEKEZAJI wa Rais Samia Suluhu Hassan kwenye kuimarisha huduma za afya umezifanya nchi jirani kuendelea kuja Tanzania kujifunza namna huduma za kibingwa na bobezi zinavyotolewa kwa kutumia mifumo na teknolojia rahisi.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel alisema hayo alipotembelea Taasisi yaMoyo ya Jakaya Kikwete akiwa ameongozana na Naibu Waziri wa Afya wa Malawi Dkt. Enock Phale.

Dkt. Phale aliambatana naujumbe wake kutoka Malawi ziara yao ililenga kujifunza namna huduma zaafya zinavyotolewa katika hospitali mbalimbali za umma pamoja na binafsi.

Ziara yao ililenga pia kuona namna ambavyoMalawi italeta wagonjwa hasa wenye uhitaji wa upasuaji wa moyo badala ya kuwapeleka kutibiwa India.

"Tanzania inapokea wagonjwa kutoka nchi mbalimbali za kiafrika takriban 25, hii inamaanisha kuwa nchi yetu sasa imepiga hatua kubwa katika kutoa huduma za kibingwa na bobezi katika kutibu magonjwa mbalimbali.

"Hatua hii inatokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Dkt. Mollel.

Aliongeza "Tanzania sasa imefikia kiwango cha asilimia 85 ya wataalam wazawa {wa ndani} wanaotoa huduma za upasuaji wa kufungua kifua huku asilimia 15 tu ndiyo wanatoka nje ya nchi na wanapokuja wanaacha ujuzi wa ziada kwa wataalamu wazawa.

Akizungumza, Naibu Waziri wa Afya wa Malawi Dkt. Enock Phale alisema nia yao ya kufika JKCI pia ni kujifunza namna gani Malawi itaweza kuanzisha huduma za uchunguzi na matibabu ya moyo.

"Tumekuwa tukitumia fedha nyingi kupeleka wagonjwa wanaohitaji upasuaji wa moyo nchini India, lakini tumeona Tanzania huduma hii inatolewa.

"Ndiyo maana tumeamua kuja kujifunza, kuona namna ganina sisi tunaweza kuanzisha taasisi



*Naibu Waziri Dkt. Godwin Mollel*



*Naibu Waziri Dkt. Godwin Mollel akisalimiana na Muuguzi wa Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete wakati alipotembelea akiwa ameambatana na Waziri wa Afya wa Malawi Dkt. Enock Phale.*



*Naibu Waziri Dkt. Godwin Mollel (Kushoto) akiwa na Naibu Waziri wa Afya wa Malawi Dkt. Enock Phale pamoja na ujumbe alioambatana nao wakipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).*

# KITUO CHA KUTOLEA MAFUNZO KWA NJIA YA MTANDAO CHAZINDULIWA TANZANIA

**Dar es Salaam**

KITUO cha mafunzo kwa njia ya mtandao kitakachotumika kuwajengea uwezo watumishi wa afya katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali ikiwamo UVIKO – 19, kimezinduliwa nchini.

Uzinduzi wa kituo hicho uliofanyika Julai 26, 2022 ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili ni ishara ya kuanza rasmi kwa mafunzo na huduma zake nchini Tanzania.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alizindua kituo hicho akiwa ameambatana na Mkurugenzi wa kituo cha kudhibiti magonjwa cha Marekani (CDC) Dkt. Rochelle Walensky pamoja na Balozi wa Marekani kwa Tanzania Dkt. Donald Wright.

Akiongoza uzinduzi huo, Waziri Ummy alibainisha kuna vituo nane na vituo vingine vidogo vidogo 272 ambavyo vinashirikiana katika kutoa maarifa kwa Watumishi wa Afya katika kuwahudumia wagonjwa.

Alisema, vituo hivyo vitasaidia kupata miongozo ya jinsi ya kutoa matibabu kwa wagonjwa na kupunguza Rufaa ambazo zinaweza kuepukika kwa kumhudumia mgonjwa katika kituo hicho bila kumpeleka Muhimbili.

Sambamba na hilo, Waziri Ummy, aliishukuru CDC kwa kuendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali, hususan katika kutoa mafunzo ya njia bora za kupambana dhidi ya maambukizi, jinsi ya kumhudumia mgonjwa na jinsi ya kufanya vipimo.

"Kwa niaba ya Serikali tunaishukuru CDC kwa kuendelea kutuunga mkono, kituo hiki kitatoa mafunzo ikiwemo jinsi ya kudhibiti maambukizi, jinsi ya kumuhudumia mgonjwa na jinsi ya kufanya vipimo na kugundua mgonjwa anaumwa nini.

Aliongeza "Matokea mazuri yanayopatikana kwa Watanzania kuchanja chanjo ya UVIKO – 19 ni kutokana na ushirikiano kati ya Tanzania na CDC.

Mbali na hayo Waziri Ummy alisema, kupitia ushirika huo na CDC umewezesha Serikali kupata maabara 44, kufundisha Wataalamu wa maabara takriban 556 katika maswala ya 'microbiology' and udhibiti ubora (quality management).

Aidha, Waziri Ummy aliishukuru Muhimbili, CDC na Balozi Wright kwa kuendelea kufanya kazi na Serikali hasa katika Sekta ya Afya kwa lengo la kulinda Afya za Watanzania.

# WADAU WA MAENDELEO, KUWENI NA MIRADI ITAKAYOGUSA WANANCHI MOJA KWA MOJA – DKT. MOLLEL

Mwanza

WADAU wa maendeleo wanaotekeleza miradi mbalimbali ya afya Kanda ya Ziwa nchini, wameombwa kupeleka fedha katika miradi itakayogusa wananchi moja kwa moja na si kutumia fedha kwenye warsha, semina na makongamano.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel alipozungumza na wadau mbalimbali wanaofanya kazi katika mikoa ya Kanda hiyo kikao ambacho kilifanyika Hospitali ya Rufaa ya Sekoue Toure jijini hapa.

Dkt. Mollel aliwasihi wadau hao kuiga mfano wa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alitumia fedha za UVIKO-19 Tsh. Trilioni 1.3 kuboresha huduma mbalimbali zinazogusa wanachi nchini ikiwemo huduma za afya.

"Rais Samia alipata fedha hizo kwa ajili ya kupunguza makali ya UVIKO-19, nchi nyingi zilipata fedha hizizikatumia kununua barakoa na mambo mengine lakini nchini kwetu Mhe. Rais ameelekeza fedha hizokwenda kumgusa mwananchi wa kawaida huko aliko," alisistiza.

Dkt. Mollel aliwaomba wadau hao kuendelea kushirikiana na Serikali kuhamasisha jamii kuhusu chanjo ya UVIKO – 19 na wadau hao walimuahidi kwamba hilo watalinga mkono ili nchi ifikie lengo iliyojiwekea.

Sambamba na hilo, Dkt. Mollel na wataalamu walijadili kwa pamoja kuona namna ambavyo wadau wa maendeleo wanaweza kuweka mikakati ya pamoja ya kugusa maisha ya watu.

Vile vile, alitembelea jengo jipya linalotoa huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Sekou Toure na kuona jinsi huduma hizo zinavyotolewa, aliwapongeza watumishi wa hospitali hiyo kwa huduma nzuri wanazotoa zilizopelekea kupunguza malalamiko.

> ***Rais Samia alipata fedha hizo kwa ajili ya kupunguza makali ya UVIKO-19, nchi nyingi zilipata fedha hizizikatumia kununua barakoa na mambo mengine lakini nchini kwetu Mhe. Rais ameelekeza fedha hizokwenda kumgusa...***

# TANZANIA KUTOKOMEZA UGONJWA WA USUBI IFIKAPO MWAKA 2030

Dar es Salaam

NI muhimu kuendeleza juhudi za kumezesha kinga tiba pamoja na uelimishaji jamii kuhusu ugonjwa wa Usubi ili kuweza kuutokomeza nchini Tanzania ifikapo mwaka 2030.

Yalielezwa hayo na Mkurugenzi msaidizi - Epidemiolojia kutoka Wizara ya Afya Dkt. Azma Simba wakati wa mkutano wa ushauri wa kitaalamu wa kutokomeza ugonjwa wa Usubi uliofanyika Dar es Salaam.

"Ugonjwa waUsubi unaathiri ngozi ya binadamu, mtu mwenye ugonjwa huu hupatwa na homa kali, hutokwa vipele mwilini, huhisi muwasho mkali pia unaweza kumsababishia upofu," alibainisha.

Dkt. Simba alisema ugonjwa huo huenezwa naInzi wadogo weusi ambao kitaalamu wanaitwa (blackfriars), huzaliana katika maeneo yenye misitu na maji yanayotiririka kwa kasi.

"Ugonjwa huu umeenea katika Halmashauri 29 ambapo takribani 7.02% ya watu wapokatika hatari ya maambukizi ya ugonjwa huu nchini," alibainisha

Aliongeza "Mikakati mbalimbali inafanyika nchini ikiwemo kumezesha kingatiba mara moja kwa mwaka katika baadhi ya maeneo huku mengine yakimezesha mara mbili kwa mwaka.

"Juhudi zilizofanyika hadi sasa kupitia programu maalumu ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ni pamoja na kuainisha maeneo yaliyoathiriwa na ugonjwa huu kwa kufanya tafiti na tathminikwa kushirikiana na wadau (NIMR, MUHAS, TFGH, CDC, WHO, KCMC, USAID, RTI)," alisema.

Aliwahimiza wananchi kuunga juhudi hizo zinazofanywa na Serikali ili kutimizaazma yake ifikapo mwaka 2030 ya kutokomeza ugonjwa huo.

Ikumbukwe kuwa hizi ni juhudi ambazo zinaendelea kufanywa baada ya agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kusaini azimio la Kigali mnamo 27, Januari 2022 lengo ikiwa ni kujitoa kwa 100% kuhakikisha Tanzania inatokomeza Magonjwa ya kitropiki yaliyokuwahayapewi kipaumbele (NTDs) ifikapo 2030.



*Dkt. Azma Simba*

# SERIKALI KUENDELEZA UJENZI KIWANDA CHA DAWA NA VIFAA TIBA IDOFI – MAKAMBAKO



*Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akisema jambo kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Dawa na Vifaatiba kwa wakazi wa Mji wa Makambako wakati wa Ziara ya ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitokea Mkoa wa Njombe kuelekea Iringa*

Njombe.

SERIKALI itaendelea ujenzi wa kiwanda cha uzalishaji dawa na vifaa tibakilichopo chini ya Bohari ya Dawa (MSD) katika eneo la Idofi– Makambako mkoani hapa.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Afya Mh. Ummy Mwalimu alipopewa nafasi ya kuwasalimu wananchi wa Makambako wakati wa ziara Rais wa Jamhuri wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan.

"Mh. Rais, hapa Makambako tunajenga kiwanda cha dawa na vifaa tibaambapo ujenzi hapo nyuma ulisimama kwa tunarekebisha mambo kadhaa, lakinisasa tunaendelea na ujenzi" alisema Waziri Ummy.

Aliongeza "Nimesimama hapa kuwahakikishia wana makambako, Serikali itaendeleza nakukamilisha ujenzi wa kiwanda hiki natutaleta Tsh. Bil. 17 kukamilisha ujenzi.

Alisema awali Serikali imeshatoa kiasi cha Tsh. Bil. 18 ikiwa ni kwaajili ya ujenzi wa Kiwanda pamoja na kununua baadhi ya mashine za uzalishaji nahadi kukamilika kwa kiwanda hicho kutagharimu kiasi cha Tsh. Bil. 35.

"Kiwanda hicho kitazalisha dawa za vidonge (Tablets) dawa za maji (Syrup) pamoja na mipira ya mikono (Gloves) huku kikitarajiwa kutengeneza fursa za ajira kwa watu zaidi ya 200," alibainisha.

# HUDUMA ZA WAJAWAZITO NA WATOTO WACHANGA KUBORESHWA KWA TSH. BIL. 17

Tanga

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya imepata ufadhili waTsh. Bil. 17 kutoka Mfuko wa Dunia wa Ufadhiliwa Huduma za Afya kwa ajili ya kuboresha huduma za wajawazito na watoto wachanga nchini ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Yalibainishwa hayo naWaziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu hivi karibuni akiwa Mkoani Tanga katika kikao kazi na wadau wa Afya kutoka Mfuko huo.

Alisema fedha hizo zitatumika kununua vifaa vya teknolojia, kuwajengea uwezo watoa huduma za afya madaktari, wauguzi, wakunga na watalaamu mbalimbali wanaohudumia wakina mama wajawazito pamoja na watoto wachanga.

Alisema vifaa hivyo mama mjamzito atavalishwa na vitaweza kusoma mapigo ya moyo ya mama mjamzito na mtoto aliyeko tumboni na vitasaidia kujua maendeleo ya mtoto na mama mjamzito," alisema Waziri Ummy.

Alibainisha kwamba, awali mradi huo umetekelezwa katika mikoa mitano hapa nchini mbayo ni Manyara, Mwanza, Tabora ,Geita na Shinyanga katika hospoitali 150.

"Katika awamu ya kwanza mradi huu umeonesha matokeo chanya kwa kupunguza vifo vya mama na mtoto mchanga ambapo asilimia 25 vifo vitokanavyo na uzazi na asilimioa 50 watoto wachanga," alisema Waziri Ummy.

Alisema utekelezaji wa mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na hospitali ya Lutheran ya Hydom iliyopo mkoni Manyara

Alisisitiza dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassani ni kuokoa maisha ya watoto wachanga pamoja na mama wajawazito

Akizungumza, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Mama na Mtoto Dkt. Ahmad Makuwani alisema lengo la utekelezaji wa mradi huo ni kuhakikisha wakinamama wajawazito na watoto wachanga wanakuwa na maisha bora hapa nchini.

"Vifo vya mama mjamzito na watoto wachanga kwa Tanzania bado nijanga kubwa hivyo bado tunakazi kubwa ya kuhakikisha tunazidi kupunguza vifo hivi nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji kutoka Hospitali ya Hyidom iiliyoko mkoani Manyara Dkt. Paschal Mdoe alimshukuru Waziri Ummy kwa ushirikiano aloutoa kwa hospital hiyo kutekeleza mradi huo katika mikoa mitano na kuleta matokeo chanya.

# TANZANIA NA UTURUKI KUANZA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA MASHIRIKIANO KATIKA SEKTA YA AFYA

Ankara, Uturuki

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Prof. Abel Makubi na Naibu Waziri wa Afya wa Uturuki Dkt. Tolga Tolunary wamekutana na kufanya mazungumzo ya namna ya kuanza mara moja utekelezaji wa Mkataba wa mashirikiano katika sekta ya afya yaliyosainiwa mwaka 2017.

Majadiliano hayo yalfanyika mwanzoni mwa mwezi Agosti , 2022 katika ofisi za Wizara ya Afya jijini Ankara, Uturuki.

Maeneo mbalimbali ya ushirikiano yalijadiliwa ikiwemo mafunzo ya kibingwa na ubingwa ubobezi kwa wataalam wa kada mbalimbali za Afya, matibabu yasiyopatikana nchini Tanzania, uwekezaji wa Hospitali, viwanda na vifaa tiba nchini Tanzania, mageuzi ya mfumo wa TEHAMA wa taarifa za afya za wananchi wote unavyotumika nchini humo.

Katibu Mkuu pamoja na ujumbe aliombatana nao walipata fursa ya kuelezwa kuhusu mageuzi yaliyofanyika kwa miaka ishirini sasa katika mfumo wa sekta ya afya na uendeshaji wa bima ya afya kwa wote unavyotekelezwa nchini Uturuki.

Aidha, uzoefu ulitolewa wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuwa na e-Database ya wagonjwa wote nchini humo, utunzaji na usafirishwaji wa kumbukumbu zao (vipimo, magonjwa, dawa) kutoka hospitali moja kwenda hospitali nyingine na utambuzi, ufatiliaji(tracking) na udhibiti wa dawa katika



supply chain kuanzia ngazi ya utengenezaji/uingizaji mpaka kwa mlaji (mgonjwa).

Vilevile, Katibu Mkuu na ujumbe wake walielezwa kuhusu mfumo unaotumiwa na Wizara ya afya kwenye huduma za dharura na majanga ambapo magari yote ya dharura yanaratibiwa kutoka vituo mbalimbali katika kituo kikuu kilichopo wizarani pamoja na uwepo wa mfumo unaofuatilia magari ya kubeba wagonjwa (ambulances) nchi nzima.

Viongozi hao walikubaliana kuundwa kwa kamati maalum ya kiutendaji itakayoratibu makubaliano yaliyofikiwa na kuweka mfumo wa tathimini na ufuatiliaji wake.

Katika ziara hiyo, Katibu Mkuu pia aliambatana na Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Uturuki Mhe. Hassan Mwamweta na kutoa salaam za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu kwa Serikali ya Uturuki.



# WASINDIKIZAJI/WASAMBAZAJI MAZIWA MBADALA NA VYAKULA VYA WATOTO ZINGATIENI SHERIA

Ikungi

SEKTA binafsi, wasindikaji, wasambazaji na wauzaji wa maziwa mbadala na vyakula vya watoto wameagizwa kuepuka matangazo ya bidhaa zao ili kuzingatia sheria na kanuni ya kudhibiti uuzaji na usambazaji wa maziwa na vyakula vya watoto wachanga na wadogo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu Mhe. Mwanaidi Khamis wakati akiongea na wananchi wa Halmashauri ya Ikungi, Mkoani Singida katika uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama kwa watoto duniani.

"Mnapaswa kuzingatia Sheria na Kanuni ya Kudhibiti Uuzaji na Usambazaji wa Maziwa na Vyakula vya Watoto wachanga na wadogo kwa kuepuka utoaji wa matangazo, ushawishi na kufanya promosheni ya maziwa mbadala na vyakula vya watoto wachanga kwenye vyombo vya habari au katika maeneo yoyote".

Aidha, alisema Viongozi wa kijamii wakiwemo Viongozi wa Dini na Siasa, watu maarufu wenye ushawishi katika jamii, wasanii na wanamichezo wana wajibu wa kuhamasisha jamii kuhusu unyonyeshaji wa maziwa ya mama".

Naibu Waziri huyo aliwataka wasambazaji na wasindikizaji wa maziwa mbadala na vyakula vya watoto kutafuta na kusambaza taarifa sahihi zinazohusu unyonyeshaji na lishe na kuepukua kusambaza taarifa au imani potofu zinazoathiri unyonyeshaji.

Hata hivyo alitoa rai kwa sekta ya viwango na udhibiti ubora wa vyakula, wanataaluma na taasisi zinazosimamia sheria zinazohusu vyakula vya watoto kuendelea kufanya tafiti na ufuatiliaji wa kina wa taratibu za uuzaji na usambazaji wa maziwa na vyakula vya watoto wachanga na wadogo ili kusaidia kuwalinda watoto hao dhidi ya athari wanazoweza kuzipata kutokana na kutumia bidhaa zisizokuwa na ubora na pia kulinda na kuendeleza unyonyeshaji watoto maziwa ya mama.

"Ujumbe wa wiki ya unyonyeshaji mwaka huu inayosema "Chukua hatua endeleza unyonyeshaji, Elimisha na toa msaada" unatukumbusha sote tuna wajibu wa kuwawezesha wanawake waweze kunyonyesha watoto wao maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo baada ya kujifungua".

Wakati huohuo Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida ambaye ni Mganga Mkuu wa Mkoa Dkt. Victoriana Ludovick alisema asilimia 93.4 ya akina mama na walezi katika Mkoa huo wamepatiwa elimu ya unyonyeshaji pia moja ya mikakati ya Mkoa ni suala la lishe kupewa kipaumbele na shughuli za lishe zinajumuishwa kwenye mpango kabambe wa Halmashauri.



# KILA MTU ATIMIZE WAJIBU WAKE ILI KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA- PROF. MAKUBI

Dodoma

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Prof. Abel Makubi ametoa wito kwa Wataalamu wa afya wote nchini kutimiza wajibu wao katika maeneo yao ya utendaji ili kuboresha huduma kwa wananchi wanaoenda kupata huduma.

Prof. Makubi alitoa wito huo katika kikao na Waganga Wakuu wa Wilaya, Halmashauri na Wafawidhi kilichofanyika kwa njia ya mtandao (zoom), ambapo Wakurugenzi kutoka Idara na vitengo mbalimbali vya Wizara ya Afya na TAMISEMI walishiriki pia.

"Nitoe wito kwenu, kila mtu atimize wajibu wake katika utendaji ili kuleta matokeo chanya katika Sekta ya Afya, hili liendane na ubunifu na uchapaji kazi ili tuone mabadiliko katika vituo vyenu vya utoaji huduma."Alisema Prof. Makubi.

Sambamba na hilo Prof. Makubi alisema, Wizara imejipanga kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa 'Clinical Audit' katika ngazi ya utoaji huduma kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya, ili kuboresha huduma na kuleta matokeo kwa wananchi.

Aidha, Prof. Makubi, aliwataka Wataalamu wa afya kufuata misingi, miongozo na taaluma zao wakati wa utoaji huduma ikiwemo matumizi ya lugha kwa wateja wanaofika kupata huduma jambo litalosaidia kuondoa malalamiko kwa wananchi yanayoweza kuzuilika.

"Hakuna kitu kinachotia hasira kama vitu vidogo vidogo kushindwa kufanyika katika maeneo ya kutolea huduma, mfano suala la lugha mbaya kwa wananchi wanapoenda kupata huduma, hii ni lazima muifanyie kazi." Alisema.

Pia, Prof. Makubi aliwataka Wataalamu hao kusimamia huduma za mama na mtoto katika maeneo yao ili kuondoa changamoto zinazoweza kuzuilika ikiwemo kuondoa vifo vya mama wajawazito vinavyoweza kuzuilika.

Kwa upande mwingine, amewaagiza kusimamia vizuri fedha za Wadau na za Serikali zinazopelekwa katika vituo vyao ili zilete tija ya kuwahudumia wananchi katika maeneo ya mbalimbali nchini.

Naye, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Afya OR-TAMISEMI Dkt. Grace Magembe amesema katika bajeti ya TAMISEMI 2022/2023 imeweka kipaumbele kikubwa kwenye vifaa tiba, kwenye suala la utumishi, kujenga na kukarabati hospitali mpya za Wilaya na Zahanati lengo ni kuboresha huduma kwa wananchi.

Dkt. Magembe amesisitiza pia ushirikiano katika utendaji kazi kwani lengo ni kuboresha utoaji huduma kwa wananchi, hasa katika wakati wa mapambano dhidi ya magonjwa ya mlipuko, huku akisisitiza ushirikiano na Sekta nyingine katika kuboresha Sekta ya Afya.

Hata hivyo, Dkt. Magembe amewashukuru Wataalamu wote kwa kuendelea kujitoa katika kuwahudumia wananchi, huku akiwatia moyo kuendelea kujitoa katika utendaji wao.

# SERIKALI KUJA NA MIKATABA YA KUPUNGUZA VIFO VYA MAMA NA MTOTO

Singida

MGANGA Mkuu wa Serikali Dkt. Aifello Sichalwe alisema, Serikali kupitia Wizara ya Afya na OR-TAMISEMI imejipanga kupunguza vifo vya Wajawazito na watoto kupitia mikataba itakayobeba viashiria vya Wajawazito na lishe inayotarajiwa kusainiwa na Wakuu wa Mikoa.

Dkt. Sichalwe alisema hayo katika kikao cha Wadau wa Sekta ya Afya kwenye eneo la mama na mtoto pamoja na Lishe kilichofanyika Mkoani Singida.

"Tumekubaliana kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais aliyoyatoa ya kuja na mkataba mmoja ambao utakuwa umebeba viashiria vya utendaji vya akina mama wajawazito pamoja na masuala ya Lishe ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kupambana dhidi ya vifo vya Wajawazito na watoto wachanga". Alisema Dkt. Sichalwe

Aliendelea kusema kuwa, pamoja na hayo Serikali kwa kushirikiana na wadau imekubaliana kuanza kutekeleza matumizi ya kanzi data, itakayotoa fursa ya kujua viashiria vya hatari vya mjamzito endapo anavyo kutokana na maswali atayoulizwa na Mtaalamu wa afya.

Sambamba na hilo Dkt. Sichalwe alisema, kwa upande mwingine Serikali kwa kushirikiana na wadau wamekubaliana utekelezaji wa azimio la vikao vya kujadili vifo vya mama na mtoto vilivyoanzishwa na Wizara ya Afya kikanda.

Aidha, Dkt. Sichalwe alieleza kuwa, kwa pamoja kama Wadau wa Sekta ya Afya wamekubaliana kutekeleza mfumo wa kusimamia magari ya kubebea Wajawazito (M-MAM) unaorahisisha mfumo wa rufaa nchini kama sehemu nyingine ya mkakati wa kupambana dhidi ya changamoto ya vifo vya Wajawazito na watoto.

Mbali na hayo, Dkt. Sichalwe aliwashukuru Wadau waliojitokeza katika kikao hicho cha Kimkakati na kuweka wazi kuwa, maazimio yote ya kikao hicho yatawasilishwa kwenye uongozi wa Wizara ya Afya na TAMISEMI kwaajili ya utekelezaji na Wadau wote walioshiriki kikao hicho na wasio shiriki watakuwa katika utekelezaji.

Hata hivyo, aliweka wazi kuwa, wamekubaliana kuleta mipango yao, namna walivyotekeleza na changamoto wanazokutana nazo wakati wa utekelezaji wa mipango hiyo na wanaishauri nini Serikali ili kwa pamoja kuona namna gani wanaweza kushirikiana kuzitatua kwa lengo la kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya mama na mtoto katika jamii.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Dkt. Ntuli Kapologwe alisema, katika kikao hicho wamepitia viashiria mbalimbali vinavyolenga masuala ya mama na mtoto ambavyo vitasaidia kuongeza uwajibikaji kwa viongozi mbalimbali ngazi ya Mkoa na kupima matokeo ya uwajibikaji huo kwa kupungua kwa vifo vya Wajawazito na watoto.

Pia, Dkt. Ntuli alisema kuwa, Serikali ilifanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ambapo vituo vya afya 650 ambavyo vinatoa huduma za upasuaji vimejengwa, huku hospitali mpya za Halmashauri 130 zikijengwa, hivyo uwekezaji huo ni lazima uende sambamba na huduma bora zitazosaidia kupungua kwa vifo vya Wajawazito na watoto.

"Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu, katika kipindi cha miaka mitano vituo vya afya 650 vinavyotoa huduma za upasuaji, sambamba na hilo hospitali mpya za Halmashauri 130, sasa uwekezaji huo lazima uende sambamba na huduma." Alisema Dkt. Ntuli.

# UGENI WA MTENDAJI MKUU WA GLOBAL FUND NCHINI TANZANIA













# HUDUMA JUMUISHI ZA TIBA ASILI NA TIBA ZA KISASA ZIMEANZA KUTOLEWA NCHINI

Morogoro

Serikali imeanza utoaji wa huduma jumuishi za tiba asili na tiba za kisasa katika vituo vya Momela Wilaya ya Meru mkoani Arusha na Maibong-SukiDar Magomeni katika jiji la Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dkt. Kusirye Ukio wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya Tiba Asili ya Mwafrika akimwakilisha Waziri wa Afya Mhe.Ummy Mwalimu yaliyofanyika Mkoani Morogoro.

Dkt.Kusirye alisema kuwa kuanzishwa kwa huduma hizo ni mafanikio makubwa kwani tangu UHURU wa nchi za kuboresha na kuendeleza huduma za tiba asili.

"Miongoni mwa mafanikio mengine ni tiba asili kutambuliwa katika Sera ya Afya,kutungwa kwa sheria ya Tiba Asili/Mbadala,kanuni na miongozo mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa tafiti za tiba asili zinazofanywa na vyuo vikuu vya Serikali"Alisema

Aidha, alisema mchango wa Tiba Asili umedhihirika zaidi wakati wa mapambano ya UVIKO-19 na kwamba viongozi na Serikali za Kiafrika zinawajibika kuona umuhimu wa kuboresha tiba hiyo katika mapambano ya adui maradhi.

"Huduma za tiba asili zilitumika wakati wa UVIKO-19 na zilifanya kazi kubwa sana kuwahudumia wahitaji ambapo dawa takribani 21 za asili zilitumika,kutokana na hilo Watanzania wamekuwa na imani kubwa na huduma za tiba asili"Aliongeza

Hata hivyo amesema Tanzania suala la kuendeleza huduma za tiba asili ni mojawapo ya kipaumbele na moja ya vipaumbele katika Ilani ya CCM ambayo kwayo Serikali itapimwa.

Kwa upande mwingine aliwataka Waganga wa Tiba Asili kutengeneza dawa zenye ubora na kuhakikiwa na Mamlaka zinazotambulika ikiwa pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu usalama wa dawa zao."Dawa zilizothibitishwa kuwa zina usalama kwa kiwango kinachokubalika ndizo zisajiliwe kwenye Baraza la TibaAsili/ Mbadala".

Pia aliwataka Wanganga wa tiba asili kuacha kuchanganya dawa za kisasa kwenye dawa zinazotengenezwa na kuuzwa kwa wahitaji na kuongeza kuwa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na vyuo inaendelea kufuatilia dawa zote za tiba asili zilizopo sokoni na dawa yoyote itakayokutwa imechanganywa na dawa za kisasa hatua kali zitachukuliwa kwa mmiliki wa dawa husika.

Naye, Mkurugenzi wa Uzamili na Utafiti kutoka SUA Prof. Esron Karimuribo alisema Tanzania ina mazao mazuri yanayofanya vizuri, yamethibitishwa ubora katika tiba na kuhakikiwa yanafanya vizuri.

Alisema SUA inaendelea kutoa elimu wa wataalamu wa tiba asili na kwa kuanza wamekuja na utaalamu wa vifungashio kwa dawa hizo pamoja na utoaji wa dozi kamili ili kupata matokeo mazuri.

Wakati huohuo Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Tiba Asili/Mbadala Bi. Elizabeth Lema amesema kutokana na kutatua changamoto za Baraza hilo hivi sasa wamewekamata vishoka na matapeli wanaopita kuwasajili waganga hao na hatua kali za kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

Bi.Lema alivihimiza vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuacha matangazo yasiyo na Vibali kutoka Baraza hilo na kwamba Baraza litaendelea kutoa elimu ili kuwa na wigo wa kuzidi kutoa tiba za Asili nchini.






*Baadhi ya wadau wakimsikiliza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dkt. Kusirye Ukio wakati wa kilele cha maadhimisho hayo yaliyofanyika Mkoani Morogoro hivi karibuni.*

*Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dkt. Kusirye Ukio akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya Tiba Asili ya Mwafrika akimwakilisha Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu yaliyofanyika Mkoani Morogoro hivi karibuni.*

# TANZANIA ITAZIDI KUKABILI SARATANI KWA VIFAA TIBA VYA KISASA, ELIMU YA KINGA – WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA

> *Kati ya wagonjwa tuliowapokea na kuwahudumia mwaka 2021 wanawake ni 70% na wanaume ni 30%. Ni tofauti na ilivyokuwa awali, wagonjwa wengi walikuwa ni wale wenye saratani zinazotokana na maambukizi ya virusi*

UGONJWA wa saratani bado ni tishio duniani, Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Saratani (IARC) inaeleza kuna zaidi ya watu milioni 43.8 wanaishi na saratani.

Takwimu za IARC zinaeleza kila mwaka kuna wagonjwa wapya milioni 18.1 wa saratani kila mwaka, duniani.

Taasisi hiyo iliyo chini ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaeleza kati ya hao, wagonjwa milioni 9.6 hufariki kila mwaka hiyo ni sawa na 50% ya wagonjwa wote wanaogundulika na saratani duniani.

WHO inaonya ikiwa mataifa hayatachukua hatua madhubuti za kinga, uchunguzi wa mapema na tiba stahiki tatizo litazidi kuongezeka, idadi ya wagonjwa wapya huenda ikafika milioni 24 ifikapo 2035.

Kulingana na Shirika hilo la Umoja wa Mataifa, inakadiriwa ongezeko kubwa litakuwa katika ukanda wa nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania.

Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya 42,060 wa saratani kila mwaka, inabainishwa hivyo na IARC katika matokeo ya tafiti yake ya mwaka 2018.

Ripoti hiyo inachambua zaidi kwamba katika kila watu 100,000 watu 76 wana saratani na kila mwaka takribani wagonjwa 28,610 sawa na 68% hufariki dunia kutokana na ugonjwa huo nchini Tanzania.

"Tumeshuhudia ongezeko la wagonjwa wa saratani ndani ya kipindi cha miaka 10 sasa, mwaka 2021 pekee tumeona wagonjwa wapya 8,000 na wa marudi ya kliniki 68,000," anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dkt. Julius Mwaiselage.

Kwa mujibu wa Dkt. Mwaiselage, takwimu za ORCI zinaonesha saratani zinazoathiri wanaume zaidi ni ya tezi dume, koo, utumbo mkubwa na mdogo na ile ya mdomo na kinywa.

Kwa upande wa wanawake inayowaathiri zaidi ni saratani za mlango ya kizazi, matiti na koo huku pia wakiathiriwa zaidi na saratani nyinginezo ikiwamo ya utumbo mpana, njia ya chakula, ngozi na damu.

"Kati ya wagonjwa tuliowapokea na kuwahudumia mwaka 2021 wanawake ni 70% na wanaume ni 30%," anabainisha.



Waziri wa Afya Ummy Mwalimu anasema ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani hivi sasa ni kwa sababu ya mtindo wa maisha usiozingatia lishe bora na kutokufanya mazoezi.

"Ni tofauti na ilivyokuwa awali, wagonjwa wengi walikuwa ni wale wenye saratani zinazotokana na maambukizi ya virusi.

"Sasa hivi, ongezeko la wagonjwa wa saratani pamoja na magonjwa mengine yasiyoambukiza (moyo, shinikizo la damu, kisukari, kiharusi nakadhalika) chanzo ni mtindo mbovu wa maisha usiozingatia afya bora.

"..., kama kutokufanya mazoezi (tabiabwete), unene uliokithiri, matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya pombe kupita kiasi, ulaji usiofaa yaani vyakula vyenye mafuta mengi, chumvi na sukari nyingi, kutokula mbomboga na matunda," anasema.

Anasema kutokana na hali hiyo, Serikali imeimarisha huduma za kibingwa katika hospitali sita za Rufaa za Kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) za uchunguzi na tiba.

"Tumeongeza wataalamu, miundombinu na vifaa tiba," anasisitiza na kuongeza "Saratani ni ugonjwa unaoathiri watu wa rika na jinsia zote watoto, watu wazima, wanawake na wanaume.

Anasema Tanzania imetunga sheria mbalimbali , miongozo na mikakati ya udhibiti wa vihatarishi ili kuweza kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.

"Theluthi moja ya Saratani zinaweza kutibika endapo mgonjwa atabainika mapema, ni muhimu kila mmoja kuchunguza afya yake mara kwa mara.

"Ili kutambua hali yake ya ki-afya, akitambuliwa mapema kuwa na saratani, akipata tiba stahiki na kuzingatia ushauri unaopewa na wataalamu wa afya, inatibika na kupona," anasisitiza.

Saratani ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza yanayogharimu mno Taifa, yakiathiri maisha ya watu wengi wa rika zote, uchumi na hata kusababisha vifo.

Julai 31, 2022 viwanja vya Jamhuri Jijini Dodoma, Ocean Road iliyo chini ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Benki ya NBC walifanya matembezi ya hisani (NBC Dodoma Marathon) kwa lengo la kukusanya fedha ili kuchangia matibabu ya wagonjwa wa saratani ya kizazi wanaotibiwa hospitalini hapo.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anasema ni muhimu wadau wengine ikiwamo taasisi za umma na za binafsi kuendelea kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya saratani hususan hiyo ya kizazi ili kuokoa maisha ya wanawake.

"Kama wanavyosisitiza wataalam wetu wa afya, saratani ya shingo ya kizazi inatibika na inaweza kuepukika endapo itatolewa elimu ya kutosha inayosisitiza kupima afya zao mara kwa mara ili kupata tiba stahiki," anatoa rai.

Anaongeza "Saratani ya shingo ya kizazi inagharimu maisha ya wanawake nchini, kati ya waliochunguzwa saratani ya kizazi na matiti mwaka 2019 wanawake 364 walikutwa na dalili za awali na wengine 26 waligundulika tayari ni wagonjwa.

"Naipongeza NBC kwa jitihada zake katika kuchangia upimaji na matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake nchini kwa kutoa shilingi milioni 200 zilizopatikana kutokana na mbio hizo.

Anaongeza "Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, imeendelea kufanya maboresho makubwa katika utoaji wa huduma za matibabu

